**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0688154873**

**Makamu Mkuu wa Shule. 0757504422/0754641005**

**Matron/Patron: 0757019684/0763338555**

**SHULE YA SEKONDARI NAMWAI**

**S.L.P 174**

**SIHA KILIMANJARO**

**TAREHE JUNE 2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**

**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NAMWAI HALMASHAURI YA SIHA MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Namwai ipo umbali wa kilomita 16 kutokea mji mdogo wa **Sanya Juu**. Ukitokea **Moshi** mjini unapanda magari yanayo elekea **Sanya Juu** kwa gharama ya shilingi **3,000/=** (Kwa wanaotokea Arusha Mjini wanashuka kituo cha mabasi **Boma Ng'ombe** na kisha kupanda mabasi yanayoelekea Sanya Juu kwa gharama ya shilingi 1500/=). Kutoka Sanya Juu stendi unapanda magari yanayoelekea **Ngare - Matadi** na kushuka kituo cha **Shule ya Sekondari Namwai** kwa gharama isiyopungua shilingi 1500/= kwa usafiri wa Noah au daladala..

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14 Agosti 2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13 Agosti 2023. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31 Agosti 2023**



Scanned with CamScanner

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni,

A) sketi ndefu 2 rangi ya **kijani kibichi (dark green)** mshono wa rinda box urefu wa kufikia kifundo cha mguu kwa Wasichana.

B) Suruali 2 rangi ya **kijani kibichi (dark green)** mshono wa marida kwa Wavulana (zisiwe za kubana)

C) Rangi ya Hijab (kijuba) ni **nyeupe** kwa darasani na rangi ya **damu ya mzee (marron)** kwaajili ya kushindia ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama);

ii. Sare ya Michezo ni

A) Tshirt ya jezi nyeupe, sketi moja nyeusi mshono wa solo, raba za michezo na ***skintight mbili ndefu nyeusi*** kwa **wasichana wa PCB na** tshirt ya jezi ya blue, sketi moja ya nyeusi mshono wa solo, raba za michezo na ***skintight mbili*** ndefu nyeusi kwa wasichana wa **PCM**

B) Tshirt ya jezi na bukta nyeusi zenye strips nyeupe kwa pembeni na viatu vya michezo kwa **wavulana wa PCB** na, tshirt na bukta ya jezi za blue zenye strips nyeupe kwa pembeni, viatu vya michezo kwa **Wavulana wa PCM**

iii. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

iv. Track-suit nzito rangi ya kijani iliyokolea isiyobana yenye strips nyeupe pembeni

v. Soksi jozi tatu au zaidi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta ni rangi ya kijani kibichi (dark green) mshono wa V shingoni ;

viii. Tisheti (T-shirt) rangi ya kijivu iliyokolea (grey) kwa darasani. Inapatikana shuleni kwa sharama ya shilingi 20,000/= pamoja na nembo.

ix. Nguo za kushindia

A) Kwa wavulana **ni Suruali mbili za draft kubwa rangi ya kijani** na tshirt 2 za rangi ya damu ya mzee iliyokolea (maroon) aina ya form six Isiwe na maandishi, alama au rangi yoyote ya ziada.

B) Kwa waasichana ni Gauni mbili **za kitambaa kizito cha draft ndogo za rangi ya kijani** mshono wa solo. Ziwe ndefu kufikia kisigino cha mguu

C) Sweta/koti mbili nyeusi nzito zisizo na maandishi au alama nyingine yoyote kwa ajili ya kushindia wakati wa baridi. (zisiwe refu)

**2:2) Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

I. Madaftari saba ***counter books Quire 3/4*** na daftari ndogo (Msomi) saba za mazoezi (**yanapatikana kwenye duka la shule**)

II. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka **(pesa hazipokolewi);**

III. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology na Scientific calculator ***fx992*** na kuendelea

IV. Godoro la futi mbili na nusu kwa sita . (**hazikodishwi shuleni)**

V. Mashuka na foronya Jozi 2 (rangi ya pink kwa wasichana na blue kwa wavulana ), blanket 1 zito, foronya ya godoro 1 pamoja na chandarua 1.

VI. Nguo za ndani za kutosha;

VII. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

VIII. Ndoo 2 (1 ndogo ya lita Kumi na 1 kubwa ya lita 20) zenye mifuniko;



Scanned with CamScanner

IX. Sabuni ya maji lita 05 kwa ajili ya usafi **(kwa wote)**

X. Vifaa vya usafi
**Wasichana** waje na Kwanja/ fyekeo 1, chelewa 1, hard broom 1 na reki 1 na **wavulana** waje na jembe lenye mpini 1, squeezer 1, fagio la nje 1 na softbroom 1 .

x.Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

ADVANCED MATHEMATICS.

1. Advanced Level Pure Mathematics, Fourth Edition by C. J.Tranter
2. Pure Mathematics, by J.K Backhouse
3. Engineering Mathematics sixth edition by K. A.STROUD
4. Advanced Mathematics1-review (problems & solutions)

BASIC APPLIED MATHEMATICS:

1. Additional and Applied Mathematics by J. F.TALBERT
2. Basic applied mathematics (BAM) by Respicius Kiiza and Lugano Mwanginde

BIOLOGY

1. Biology by S.Chand
2. Biological science by D.J.Taylor
3. Biology for form V&VI by TIE
4. Biology for Advanced level, new understanding,4th Edition by Gleen & Susan Toole

CHEMISTRY

1. Conceptual Chemistry1 &2 (S. Chand)
2. Chemistry in action (Michael Fremantro)
3. Advanced chemistry by Michael Clugston, Rosalind Flemming
4. Comprehensive approach to advanced level CHEMISTRY questions with answers by Sedrick C. Magas, & Kira Ernest
5. Physical chemistry with General chemistry (Advenced) Mark Daniel Hermes Daniels.

PHYSICS

1. Advanced level physics7th Edition by Nelkon and Parker
2. Advanced physics by Sterv Adams and JonathanAllday
3. Advanced physics review
4. Principle of physics by Chand

GENERALSTUDIES

1. Understanding General Studies For Advanced Level by Bigiwamungu & Deogratius
2. Contemporary Approach for advanced level general studies notes (form 5 & 6) Nyambari Nyagwine



Scanned with CamScanner

**2:3) Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Namba ya Account ni **40101200102 NMB** Jina la account ni **NAMWAI SEKONDARI**. mwanafunzi aje na slip hakuna pesa inayopokolewa shuleni

**2:4) Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote kulingana na ratiba ya shule.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**



Scanned with CamScanner

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Uvutaji wa sigara, Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba , Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia lain au simu ya mkononi au kifaa chochote cha umeme(pasi, charger,radio) katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa, picha ya Rais na Mwenge wa Uhuru;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xvii. Kwenda kwenye nyumba za walimu na watumishi wasio walimu bila ruhusa au sababu za msingi.
xviii. Mwanafunzi wa kike kwenda kwenye mabweni ya wavulana au mwanafunzi wa kiume kwenda kwenye mabweni ya wasichana.
xix. Kutoroka au kuondoka shuleni bila ruhusa ya mkuu wa shule.

**3:3) Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**
**Saini ya Mkuu wa Shule** ……………………………………………
**Jina la Mkuu wa Shule ANNA J. URASSA**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NAMWAI

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ……………………………………

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi**

Scanned with CamScanner

husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

KWA MAWASILIANO ZAIDI

- Mkuu wa shule 0688154873
- Makamu Mkuu wa Shule 0757504422/0754641005
- Mwandamizi Taaluma 0710830315
- **Matron/Patron: 0757019684/0763338555**



Scanned with CamScanner

# TH E PRESDENT'S OFFICE
# REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
# ……………………… HOSPITAL/DISPENSARY
# MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a medical Officer)

Students's full name

……………………………………………………………………………………………

AGE…………………………………SEX……………………………………………………

Blood count (red and white)

……………………………………………………………………………………………

Stool examinations

……………………………………………………………………………………………

Urinalysis

……………………………………………………………………………………………

Syphilis test

……………………………………………………………………………………………

T.B.test

……………………………………………………………………………………………

Eye test

……………………………………………………………………………………………

Ears

……………………………………………………………………………………………

Chest

……………………………………………………………………………………………

Abdomen

……………………………………………………………………………………………

Spleen

……………………………………………………………………………………………

Additional information or any other difficultues:

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

I certify that the above IS OR IS NOT fit to pursue further studies.

Signature …………………………Designation ………………………………………………..

Station ……………………………………………STAMP…..…

Date: …………………………………………..………



Scanned with CamScanner

## SHULE YA SEKONDARI NAMWAI

## FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUTII SHERIA/KANUNI ZA SHULE

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Jina la mwanafunzi | | | jinsi | dini |
| | | | | | |
| 2. | Tarehe na mahali pa kuzaliwa | Tarehe | Mkoa | Wilaya | Mtaa/kijiji |
| | | ……/……/…… | | | |
| 3 | Mahali unapotoka/unapoishi | Mkoa | Wilaya | Kata | Kijiji/mtaa |
| | | | | | |
| 4. | Je wazazi wako wapo hai? | ndiyo | hapana | Taja hali ya uyatima (Mzazi mmoja au wote wawili) | |
| | | | | | |
| 5. | Taarifa ya wazazi/walezi | Jina la mzazi/mlezi | Makazi (mtaa na mkoa) | Kazi/shughuli anayofanya mazazi/mlezi | Namba za simu zinazopatikana za mzazi/mlezi |
| | | | | | |
| | | | | | |
| 6. | Taarifa shule uliyohitimu awali | Jina la shule na | Mahali shule ilipo | Madaraka uliyoshika/kuhudumu na kwa muda gani | |
| | | | | | |

MKATABA WA KUTII SHERIA/KANUNI ZA SHULE NA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI;

Mimi ………………………………………………………… mwanafunzi mchepuo wa ……… katika shule ya Sekondari Namwai. Nimesoma na kuelewa vizuri kanuni/sheria za shule (UK-6 na 7)kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, ninaahidi ya kuwa nitazingatia na kuzifuata vyema kanuni na sheria zilizoanishwa na kwamba adhabu kali itachuliwa dhidi yangu nikifanya kinyume.

Sahihi ya mwanafunzi........................................................ tarehe...........................

FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE

Mimi………………………………mzazi wa mwanafunzi ………………………………………….mchepuo wa ……… katika shule ya Sekondari Namwai. Nimesoma, nimeelewa na nakubaliana na sheria kanuni na maelekezo mengine yakayotolewa na shule.

Sahihi ya mzazi........................................................ tarehe.........................

Scanned with CamScanner